MTIHANI WA MWIGO –INTERZONAL

102/2
KISWAHILI
KARATASI 2
(UFAHAMU, UFUPISHO, MATUMIZI YA LUGHA NA ISIMU JAMII)
JULAI/AGOSTI-2009
MUDA: SAA 2 ½

UFAHAMU
Soma kifungu hiki kasha ujibu maswali.

Ni jambo la busara kwetu vijana kusikiza mashauri tunayopwewa na watu wazima kam vile wazazi na walimu kwani wametuzidi umri. Ama kwa hakika lolote lile wakuu wetu hutuambia yafaa tulizingatie tuseje kufikwa na balaa.
Matata alikuwa kijana mwenye sura na tabasamu nzuri. Aliweza kuwavutia wengi has wasiomjua. Hata hivyo hakuna kizuri kisicho na dosari. Matata alikuwa na tabia mbaya isiyopendeza wengi. Alikuwa mkali kama pilipili na mkaidi kama mkia wa nguruwe. Tabia yake iliwashinda wengi.

Shuleni, alivuta bangi na nyumbani alikuwa haambiliki. Aliwatukana wazazi wake hadharani. Shuleni aliwapiga na kuwaibia wanafunzi wenzake.

Mwishowe, tabia yake ilizidi na siku moja akavunja duka akiwa na vijana wengine. Alishikwa na kufungwa miaka mitano ngerezani.

Maswali:
(a) Toa kichwa mwafaka cha habari hii. (alama 3)
(b) Kwa nini maneno ya watu wazima yana umuhimu kwetu hasa vijan? (alama 5)
(c) Ni mambo gain mabaya matata alifanya (alama 4)

(i) nyumbani?
(ii) Shuleni?

(d) Ni nini kilitokea baadaye? (alama 4)
(e) Katika taarifa pilipili inatumiwa kama nini? (alama 4)

2. MUHTASARI
Soma makala yafuatayo kasha ujibu maswali.

Siku hizi elimu kwa motto wa kike imeguduliwa kuwa akiba ya kipekee ambayo nchi yaweza kujivunia. Elimu kwa wasichana hutoa mchango mkubwa katika upanuzi wa uchumi wan

chi na pia kupunguza na kuzuia idadi ya watoto ovyo. Aghalabo, hali ya afya na lishe bora ka motto pia huweza kudumishwa.

Ni bayana kwamba elimu imewaongezea wanwake matumaini ya kushiriki katika maswali nyeti ya kijamiii na kisiasa. Kwa hivyo, elimu kwa motto wa kike ni jambo la kuonea fahari mno, hasa katika nchi za kusini mwa jangwa la Sahara, ambako maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisisa yametatazika kutokana na idadi kubwa ya watu, ambao ni vigumu kwa serikali za hizo nchi kuwakidhi kimahitaji. Hii ni kutokana na ukosefu wa rasilimali za kutosha.
Yafaa ifahmike wazi kwamba wanawake ndio msingi thabiti wa maisha barani Afrika, hii ni kutokana na majukumu haya yote, inasikitisha kuona kwamba zaidi ya wasichana milioni thelathini kutoka katika nchi za kusini mwa jangwa Sahara wamekosa elimu.

Wachache walio na bahati ya kufika shuleni hawahudumiwi ipasavyo- jambo ambalo limesababisha nusu ya idadi ya wasichana wanaotamatisha masomo ya shule ya misingi, ikilinganishwa na asilimia hamsini na tano ya wavulana.

"Katika baadhi ya nchi, ni asilimia kumi na tano tu ya wasicha ikilinganishwa na asilimia arobaini na tano ya wavulana ndio hujiunga na shule za upili. Kwa hivyo ni wazi kwamba, pengo la tofauti za kijinsia na kielimu huzidi kupanuka katika kila ngazi ya masomo, "alifichua mmoja wa viongozi wa FaWe" katika vyuo vikuu nchini Kenya na Tanzania ni asilimia thelathini tu ya wanawake ndio hufuzu kila mwaka, ikilinganishwa na asilimia sabini ya wanaume.

Kulingana na FAWE hali ya watoto wa kike tutopiga hatua kimasomo huletwa na sababu mbali mbali za kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Moja ya sababu kuu ni umaskini, ambao umewakumba wazazi wengi hasa kwa waishio mashambani, na kuwafanya wasiwe na uwezo wa kununulia watoto vifaa muhimu vya masomo pamoja na kuwalipia karo. Jambo hili limewafanya wazazi kuwashurutisha watoto wao wa kike kuwapa nafasi wavulana ambao yamkini wanaweza kustahimili hali ngumu ya maisha wakilinganishwa na wasichana.

Vile vile imebainika wazi kwamba baadhi ya wazazi wangali wanatawaliwa na mtazamo uliopitwa n wakati, kuwa kumwelimisha msichana ni sawa na kupeleks mali hadi kwa familia nyingine, kwani kulingana na wao, punde atakapotamatisha masomo, ataolewa na hapo kuhama na mali yote. Isitoshe, katika baadhi ya jamii, msichana anasawasishwa kama chombo cha kuzaa watoto na hivyo, hastahili kuwa na sauti wala kuanya uamuzi wotote, huku wenzao wa kiume wakijihusisha katika utafiti wa matukio ya kisiasa.

Kikwazo kingine kwa elimu ya watoto wa kike ni dhuluma na unjisi wanaofanyiwa hasa sehemu za shule ambao umekuwa wa kutisha mno. Jambo hili limefanya kiwango cha elimu ya wasichana kudidimia na hata wengine kung'atuka shuleni kutokana na kushika mimba au kuugua majonjwa ya zinaa, ukiwemo ukimwi.

(a) Nchi inaweza kunufaikaje kutokana na elimu kwa wanawake?
(maneno 60-56) (alama 8)

Nakala chafu

Nakala safi

(b) Eleza vizingiti mbalimbali vinavyoathiri elimu kwa wanawake barani Afrika. (maneno 40 40-50) (alama 9)

Nakala chafu.

Nakala safi

3. MATUMIZI YA LUGHA

Kanusha sentensi hizi. (alama 2)

(a) (i) Wanasema wataondoka leo hii.

(ii) Wangefika nymbani mapema wangemptata mama yao angali hai.

(b) Unda majina kutokana na vitenzi vifuatavyo. (alama 2)

(i) Tibu

(ii) Fa

(c) Geuza sentensi hii katika hali ya usemi halisi.

(i) mwalimu alimwita juma mara mbili aende alipokuwa. (alama 2)

(d) Ziandike sentensi hizi upya kwa kufuata maagizo.

(i) Uko na pesa yoyote unikopee ili niweze kukimu mahitaji yangu. (sahihisha sentensi) (alama 2)

(ii) Mtoto aliyekuwa jikoni alkiumwa mkono na nyoka na mbwa kwa wakati mmoja . (Andika kwa udogo) (alama 2)

(e) Andika idadi ya tarakimu ifuatayo kwa maneno . (alama 2)
(i) 1,001, 101
(ii) CLIX

(e) Taja methali nyingine iliyo na maana sawa na kila moja yao uliyopewa. (alama 4)
(i) Fimbo ya mbali haiui nyoka.
(ii) Kidole kimoja hakivunji chawa.

(g) Toaneno moja kwa maelezo yafuatayo. (alama 3)
(i) mbuni huzaa
(ii) Mpunga huzaa
(iii) Mkonge huzaa

(h) Akifisha
(i)Karibu odhiambo akaitikia mbona huingii na mlango u wazi naam starehe kwenye kiti asance akajibu. (alama 2)

(i) (i) Tunga sentensi sahihi kwa kutumia alama za dukuduku.
(ii) Eleza matumizi ya "kwa" katika sentensi ifuatayo (alama 3)

(j) Tumia bishara vya kuthibitisha vya katibu. (alama 3)
(i) Unywele……..ndio ulikatika jana.
(ii) Mbwa……ndiye alikula chakula chote.
(iv) Jiwe…….lilipandwa jana.

(k) (i) Wageni ambao waliofika juzi watandoka leo. (sahihisha) (alama 1)

(L) Chakula ambacho kilipikwa ni kitamu sana(Ondoa "amba')

(m) Andika katika kauli ya kutendeana. (alama 2)

(i) mwalimu anajua hali ya mwanafunzi.

(ii) Wao wanataka kutujaribu. (alama 3)

(n) Eleza maana ya semu hizi. (alama 3)
(i) Riale kwa ya pili.
(ii) Kula chumvi nyingi

(o) Kamilisha sentensi hizi. (alama 3)
(i) Hapa_____ nyoka aliingia.
(ii) _____ndimo majangili waliwashika kafari.
(iii) Huku_____panya alikibizana na paka.

(p) Andika kinyume.
(i) mfalme mfupi mnene ameoa. (alama 2)

(r) Ainisha.
(i) Lo! Nyoka mkubwa alionekana chumbani. (alama 2)
(ii) Mama wa kambo hakunilipia karo. (Andika katika hali ya mazoea) (alama 2)

(s) Tunga sentensi sahihi kwa kutumia kinyume cha maneno yafuatayo. (alama 2)
(i) Ezeka
(ii) Oa

(t) Tunga sentensi kutofautisha vitate hivi. (alama 2)

(i) Remba
(ii) Lemba

4. ISIMU JAMII

" Toa zote mpaka sauti ya mwisho! Unasikia/ Chapuchapu ama ni kuset…

(a) (i) Hii ni lugha gain? (alama 1)
(ii) Fafanua sifa tatu za sajili hii. (alama 3)

(b) Dhana zifuatazo huleta maana gain katika mawasiliano ya jamii.
(i) lugha rasmi (alama 2)
(ii) Lugha ya taifa (alama 2)
(iii) Misimu (alama 2)